**IDARA YA SHERIA YA AMERIKA**

*Afisi ya Wakili wa Amerika*
*Wilaya ya Rhode Island*

**Kitengo Cha Haki za Raia**
**Sehemu ya Nafasi za Elimu**

USAO DJ 2016V256

CRT DJ 169-66-10

*50 Kennedy Plaza, 8th Floor*
*Providence, Rhode Island 02903*
*(401) 709-5000*
*FAX (401) 709-5001*

Septemba 15, 2021

**Kwa Barua ya Umeme**

Charles A. Ruggerio, Esq.
Labor and Employment Counsel
Deputy City Solicitor
Providence School Department
797 Westminster Street
Providence, RI 02903

Aubrey L. Lombardo, Esq.
Henneous Carroll Lombardo, LLC
155 South Main St., Suite 406
Providence, RI 02903

Kaelyn Phelps, Esq.
Legal Counsel
Rhode Island Department of Education
255 Westminster Street
Providence, RI 02903

Kuhusu: Kuendeleza Makubaliano ya Azimio za Wasomi wa Kiingereza katika shule za Umma za Providence ya 2018.

Kwa Mawakili Ruggerio, Lombardo, na Phelps:

Kama vile mnavyojua, mnamo tarehe Agosti 9, 2018, Idara ya sheria ya Amerika, ("Amerika") na Shule za Umma za Providence ("Wilaya") (pamoja, "Washiriki") zilitekeleza Makubaliano ("Makubaliano"), ambayo yanalenga kutatua mambo ya kutokubaliana na ridhaa ya Mwanafunzi wa Kiingereza wa Wilaya ("EL", Kifupi kwa Kiingereza ) kama yaliyotambuliwa na Amerika kuhusu azimio na matendo chini ya sehemu 1703(f) ya Sheria ya Nafasi Sawa Za Elimuya

1974, 20 U.S.C. § 1703(f). [1]Kuanzia wakati huo,Wilaya imefanya maendeleo ambayo yanadhihirika kwa kutimiza masharti yake kulingana na Makubaliano. Hasa, Wilaya imejitolea rasilimali kutambulisha EL, mawasiliano ya mdomo na maandishi na wazazi, ukuzaji wa kitaalam kwa waalimu na wafanyikazi, mtaala wa madarasa ya ukuzaji wa lugha ya Kiingereza, na Kiingereza kama udhibitisho wa Lugha ya Pili ("ESL", Kifupi kwa Kiingereza) kwa waalimu wake.

Hata kama maendeleo ambayo yamefanywa na Wilaya na kisha Idara ya Elimu ya Rhode Island (RIDE) yanadhihirika wazi, Wilaya bado haijatimiza masharti na nyakati zilizowekwa kutimiza masharti ya Makubaliano. Tazama, kwa mfano, Barua za Usimamizi wa Amerika kwa Wilaya zilizoandikwa mnamo tarehe Februari 21, 2019, Februari 21, 2020, na Machi 5, 2021. Katika mazungumzo na Wilaya na RIDE, yakiwemo mazungumzo yetu na Msimamizi wa RIDE, Angelica Infante-Green na Msimamizi wa zamani wa PPSD (Wilaya ya Shule za Umma za Providence), Harrison Peters mnamo tarehe Aprili 16, 2021, America ilihangaika kuhusu kutokubaliana na ridhaa.

Huo mhangaiko ni pamoja na, hata ingawa haya si yote, katika Wilaya kutowapatia Wasomi wote wa Kiingereza huduma za kutoshana zinazofaa za Kiingereza kama Lugha ya Pili na Mafunzo Yaliyolindwa na waalimu waliothibitishwa kufundisha Kiingereza Kama Lugha ya Pili, au wako njiani kutimiza uendelezaji wa umaarifa na masaa ya mafunzo ya darasani yanayohitajika na Makubaliano. Tazama Makubaliano¶¶ 8-10, 13, 18, 20-22; *pia tazama* Barua ya America kwa Wilaya ya tarehe Desemba 3, 2020 (iliyo kubali kuongeza muda wa Makubaliano kwa waalimu wamalize uendelezaji wa umaarifa uliobakiana kusaidia masaa ya mafunzo ya darasani yanayohitajika na Aya 21 ya Makubaliano kuenda mpaka Mwaka wa Shule (“SY”) 2021-22 na kupatia Wilaya muda wa kurekebisha kutokubaliana na ridhaa).

Ili kuhakikisha kwamba Wilaya imetimiza masharti yake yote, Washiriki wanakubali kwamba inabidi Makubaliano yaongezewe muda, ukifupishwa sana, mpaka Mwaka wa Shule 2022-23. Washiriki pia wanakubali kwamba kuongeza muda wa Makubaliano, nakubadilisha kidogo idadi ndogo ya mafafanuzi na ya kama inayoonyeshwa hapa chini, itawezesha Wilaya kukubaliana na ridhaa za masharti ya Makubaliano. [2] Mafafanuzi ambayo yalisahihishwa na aya zilizoko kwa hii barua zinachukua mahali pa mafafanuzi na aya zinazolingana kwa Makubaliano ya asili. Mafafanuzi na aya zingine zote kwa Makubaliano ya asili zinabaki kama masharti kwa Wilaya.

**Mafafanuzi yaliyo sahihishwa**

> **Kiingereza kama Lugha ya Pili ama ESL** ni maelezo yaliyo sahihi na dhahiri kuhusu lugha ya Kiingereza inayotoa mwelekeo wenye utaratibu na uendelezaji wakufunza lugha. Maelezo ya ESL yanahimiza kanuni za kusikiliza, kuongea, kusoma, na kuandikaza Sanii na Kisia za Kiwango cha Dunia (“WIDA”) za Kuendeleza Kanuni za Lugha ya Kiswahili iliyo chaguliwa na Idara ya Elimu ya Rhode Island (“RIDE”). ESL inafunzwa na mwalimu aliyehitimu na cheti cha Kiingereza kama Lugha ya Pili kutoka RIDE.

[1] Mnamo tarehe November 1, 2019, Idara ya Elimu ya Rhode Island (“RIDE”) ilichukuwa mamlaka juu ya Shule za Umma za Providence na, pamoja na mabadiliko mengine, ikatangaza kwamba Mkubwa wa Providence angekuwa chini ya Mkubwa wa RIDE. Katika mkutano wetu na Msimamizi Infante-Green na waakilishi wa RIDE na Wilaya wa Desemba 19, 2019, washiriki wote walikubali kwamba Makubaliano yana watilia masharti Wilaya na pia RIDE. *Tazama*¶ 48. Kwa hiyo kadiri, kumbukumbu zote za masharti ya Wilaya katika Makubaliano zinahusisha RIDE.

[2] Kwa uthabiti na udhihirisho, Washiri ikiwa liwe katarakimu ya aya, mlinganisho wa aya, na nyingi za tarehe za kutoka kwa Makubaliano ya 2018.

**Lugha Kuu** inamaanisha lugha ambazo zinaongewa zaidi katika Kiingereza kama Lugha ya Pili Wilayani kando ya Kingereza, zikiwemo Kihispania, Kiarabu, Kiswahili na Kikhmeri, pamoja na lugha zozote zinazoongewa na watu mia moja au zaidi, ambao bado wako, na wale wamesha ondoka, na bado wamesajiliwa Wilayani.

**Aya zilizosahihishwa**

Aya 9

Wilaya inakubali kuwa ESL ni somo la msingi kwa EL na itatoa ESL pamoja na masomo mengine ya msingi, isipokuwa kwamba Wilaya inaweza kutoa ESL kupitia darasa la msingi la kusoma na kuandika kwa EL tu zilizo na kiwango cha Ustadi wa Lugha ya Kiingereza ya 4-4.8 ikiwa darasa ni:

(a) kufundishwa na Mwalimu aliyethibitishwa na ESL ambaye pia amethibitishwa katika Sanaa ya Lugha ya Kiingereza, au

(b) kufundishwa pamoja na Mwalimu aliyethibitishwa na ESL na mwalimu aliyethibitishwa katika Sanaa ya Lugha ya Kiingereza ambao wana wakati wa kupanga pamoja, na ESL Mwalimu aliyehakikishiwa hutoa ELS wazi ESL. Wilaya inaweza kupanga ELs kwa ESL na kwa ESL iliyoingizwa katika ELA na (a) kiwango chao cha Ustadi wa Lugha ya Kiingereza ndani ya daraja moja au wima kwa daraja (imepungua kwa darasa mbili mfululizo katika kiwango cha msingi) au (b) mbili zinazolingana, Kiingereza mfululizo Viwango vya Ustadi wa Lugha ndani ya daraja moja. Vyama vinakubali kwamba vifungu vya vikundi chini ya aya ya 9 vinapaswa kutekelezwa kulingana na SY ya mwisho ya Wilaya 2021-22 na 2022-23 kupangilia nyaraka za mwongozo kwa shule zake za msingi, kati, na sekondari. [3]

Mwanafunzi yeyote Msomi wa Kiingereza katika shule ya katikati au ya upili ambaye kiwango chake cha Umaarifa wa Lugha ya Kiingereza hakikupitishwa kuendelea kwa kiwango kinachofuata kutoka kwa mwaka wa shule ambao umepita ( kwa mfano mwanafunzi ambaye mwisho alikuwa na Umaarifa wa Lugha ya Kiingereza wa kiwango cha 1.0 katika ACCESS na bado yuko na kiwango chini ya 2.0 katika Umaarifa wa Lugha ya Kiingereza), lakini alipita masomo ya Kiingereza kama Lugha ya Pili ya kiwango hicho, ESL, atawekwa kwa kikundi kifuatacho cha masomo ya Uendelezaji wa Lugha ya Kiingereza, ELD.

Aya 10

Kwa haraka iwezekanavyo, na isiwe baada ya mwanzo wa mwaka wa shule wa 2020-21, Wilaya itapeana muda Zaidi wa Kiingereza kama Lugha ya Pili kwa wale ambao wanakuja upya na Wasomi wa Kiingereza wa Wilaya ambao wana viwango 1 na 2 katika Umaarifa wa Lugha ya Kiingereza. Wilaya itatosheleza hili sharti la kupeana nyakati mbili za mafunzo ya Uendelezaji wa Lugha ya Kiingereza kwa wanaokuja upya na Wasomi wa Kiingereza ambao wana viwango vya L1 na L2 katika Umaarifa wa Lugha ya Kiingereza kuambatana na maandiko ya orodha ya mwelekezo wa kupanga wa Mwaka wa Shule wa 2021-2022 na 2022-2023 washule za mwanzo, za katikati and za upili za Wilaya.

Aya 11

Wazazi wakiidhinisha, kwa maandishi ya kujitakia ya kutoa lawama ambayo yatatumwa kwa wazazi katika lugha ambayo wanaielewa, kwamba hawataki watoto wao Wasomi wa

[3] Wilaya pia itatekeleza mpango wa Muundo wa Uendelezaji wa Usemi wa Lugha Mbili kulingana na maandiko ya mwisho ya orodha ya mwelekezo wa kupanga wa Mwaka wa Shule wa 2021-2022 na 2022-2023

Kiingereza wa Wilaya kupata huduma za Wasomi wa Kiingereza, Wilaya itawauliza wazazi ni kwanini wanachagua kutokuwa kwa Wasomi wa Kiingereza, wataiandika habari hii, na watafuata kanuni za kutokuwa wanafunzi wa Wasomi wa Kiingereza kama ilivyoratibiwa kwa Aya 8 ya Makubaliano, na waiarifu America kuhusu hii habari kabla ya Desemba 31, 2018, na kila mwaka baada ye mnamo July 15.

Aya 22
Katika mwanzo wa mwaka wa shule 2019-20, Wilaya itawahitaji waalimu wa kutoshawa mambo muhimu yaliyomo ya Wasomi wa Kiingereza wawe wametimiza au wawe njiani ya kutimiza mafunzo yaliyo orodheshwa katika Aya 21ili waweze kukubaliana na ridhaa ya Aya 13 na 14. "Kuwanjiani" kutimiza mafunzo kwa miaka mitatu inamaanisha kwamba waalimu ambao ni wapya Wilayani watapata masaa kumi ya uendelezaji wa umaarifa kwa malengo ya uwaalimu, na masaa matano ya usaidizi wa darasani kuhusu jinsi ya kutumia hayo malengo kila mwaka. Kwa mwaka wa shule wa 2021-2022, waalimu ambao hawako njiani kutimiza mafunzo yanayohitajiwa na Aya 21, lakini wamemaliza, kwa chini zaidi, vipindi 31 vya uendelezaji wa maarifa, na watamaliza uendelezaji wa maarifa uliobakia na masaa 15 ya usaaidizi wa mafunzo ya ndani ya darasa kabla ya mwisho wa mwaka wa shule 2021-2022, wanaweza kufundisha madarasa ya mafunzo muhimu ili kukubaliana na Aya 13 na 14. Waalimu wa mwaka wa kwanza na wa pili watachukuliwa kama "wako njiani" kama watakuwa wametimiza masaa 10 ya uendelazaji wa maarifa, na masaa tano ya usaidizi wa ndani ya darasa kwa kila mwaka wa mwaka wa shule ambao wamekuwa wakifanya kazi katika Wilaya [4]

Aya 42
Wilaya itapima nguvu ya matokeo ya kila mpango wa Wasomi wa Kiingereza wilaya nzima, ilikuona kama wamekuwa wakivishinda vizuizi vya lugha katika muda unaokubalika, nakuwawezesha wanafunzi kushiriki kwa maana na kwa usawa katika mipango yake ya elimu. Kufikia mwisho huo, Wilaya inakubali kufanya mchanganuo wa muda mrefu wa vikundi kwa miaka mitatu katikaki la mpango wake waviwango vya shule ya mwanzo, ya katikati na ya upili, kwa kutoanishana kuangalia kwa makini mambo yafuatayo ya hakika kulingana na Wasomi wa Kiingereza walioko, waliokuwa na ambao hawajawahi kuweko kwa kila mpango wa Wasomi wa Kiingereza unaotumiwa na Wilaya: matokeo ya mitihani yaliyosawazishwa, idadi ya wanaotoka, idadi ya wanaowacha, idadi ya wanaohitimu, idadi ya wanaobaki darasani, vipimo vya Umaarufu wa Lugha ya Kiingereza, nausajili kwa elimu maalum na mipango ya kujinufaisha (kwa mfano wenye vipawa, madarasa ya masomo ya hali ya juu, na madarasa ya Nafasi ambazo Zimeendelea). Katika kufanya mchanganuo huo, Wilaya itafuatilia vikundi vya Wasomi wa Kiingereza waliosajiliwa katika chuo cha watoto wadogo, darasa la tatu, darasa la sita, na darasa la tisa katika mwaka wa shule 2016-2017, na ambao watakaa kama wamesajili wakati ka Wilaya wakati wote wa haya Makubaliano. Wilaya itatumia matokeo ya mchanganuo wa muda mrefu kuarifu Wasomi wa Kiingereza kuhusu maamuzi ya mpango na kuhakikisha kwamba kila mpango wa Wasomi wa Kiingereza ambao wanatumia unaleta matokeo yaliyotarajiwa.

[4] Katika mwaka wa shule 2022-23, Wilaya itahakikisha kwamba waalimu wa mwaka wa kwanza na wa pili watapata hivi vipindi kwa utaratibu ambao, kwa karibu vile itakavyowezekana, itaonyesha mwandamano kama vile umeorodheshwa katika upeo na mwandamano wa uendelezaji wa umaarifa wa Wilaya (ule "Muundo wa PD")

Zaidi, Wilaya itamaliza mchanganuo wa muda mrefu wa kuongeza wakitumia msingi wa mwaka wa shule wa 2018-2019 nakufuatilia mambo ya hakika iliyoagiziwa hapo juu kwa aya hii kwenda mpaka mwaka wa shule 2022-23.Huu mchanganuo unaweza kutumiwa kama jambo katika kupima kukubaliana na ridhaa ya Makubaliano na utatumiwa kuarifu mpango wa Wasomi wa Lugha ya Kiingereza kuhusu maamuzi na kuhakikisha kwamba kila mpango wa Wasomi wa Kiingereza wa Wilaya unaleta matokeo yaliyotarajiwa. Washiriki wanatambua kwamba matokeo ambayo hayakuwa yametarajiwa yajangana vizuizi kwa mafundisho yaliyofuata yanaweza kutatiza matokeo ya ule utafiti wanyongeza wa muda mrefu, na washiriki wamekubali kuchukulia haya matukio maanani wanapochanganua kukubaliana na ridhaa na Makubaliano kwa Wilaya.

Kwa kutia sahihi kwa barua hii, Wahusika wanakubali kuongeza muda wa Makubaliano mpaka wakati ule Wilaya itatimiza masharti yake yaliobaki, na kupeana simulizi kamili funaisiyo na hitilafu inayo orodhesha kukubaliana na ridhaa kwake, na hayo masharti chini ya Aya 43.

Wahusika wanakubali kwamba Wilaya itapeana simulizi ya uangalifu zikiwemo habari zinazohitajika na Aya 43.A and 43.B kwa mwaka wa shule wa wakati huo mnamo tarehe Oktoba1, 2021 na Oktoba 1, 2022, na sehemu zote za Aya 43 za mwaka wa shule ambao umeisha punde tu kabla ya Julai 15, 2022 na Julai 15, 2023. Wilaya itapeana matokeo ya somo la nyongeza la muda mrefu kwa Amerika kabla ya Oktoba 15, 2023. Kufuatia kupeanwa kwa simulizi kamilifu na nyongeza ya masomo ya muda mrefu, Washiriki wanakubali kwamba Amerika itakuwa na siku, zikipunguka sana, 90 kuangalia simulizi na kusema mahanga iko ambayo yanaweza kuendeleza yale masharti ambayo hayakubaliani na ridhaa ya mahitaji ya Makubaliano zaidi.

Barua hii haitoi jukumu kwa Wilaya kwa masharti yoyote ambayo ni hakika chini ya Makubaliano, na Amerika itaendelea kuangalia Makubaliano kwa makini kuambatana na masharti yaliyoko sasa, na njia za kufanya yatimike.

RICHARD B. MYRUS
Wakili Mtendaji wa Amerika
Wilaya ya Rhode Island

______________________________
AMY R. ROMERO
Mdogo wa Wakili wa Amerika
District of Rhode Island
50 Kennedy Plaza, 8th Floor
Providence, RI 02903
Simu: (401) 709-5010
amy.romero@usdoj.gov

SHAHEENA A. SIMONS
Mkubwa
Sehemu ya Nafasi za Elimu
Kitengo cha Haki za Raia

______________________________
WHITNEY M. PELLEGRINO, Naibu wa Mkubwa
ANDREA HAMILTON, Wakili wa Mashtaka
LAURA TAYLOE, Wakili wa Mashtaka
NATANE SINGLETON, Wakili wa Mashtaka
Sehemu ya Nafasi za Elimu
Kitengo cha Haki za Raia
Idara ya Sheria ya Amerika
950 Pennsylvania Avenue, NW
Washington, DC 20530
Simu: (202) 514-4092
andrea.hamilton@usdoj.gov
*Mawakili wa Amerika*

Kwa Niaba ya Wilaya ya Shule ya Providence:

___________________________________ Tarehe: ______________________

JAVIER MONTAÑEZ, Msimamizi Mtendaji
Providence Public School District
797 Westminster Street
Providence, RI 02903

For the Rhode Island Department of Education:

___________________________________ Tarehe: ______________________

ANGELICA INFANTE-GREEN, Mwenye Amri
Rhode Island Department of Education
275 Westminster Street, 4th Floor
Providence, RI 02903